## SOMO LA SABA



# WAJIBU WAKO NI NINI?

*Tafadhali andika jina lako hapo juu kisha jaza nukuu za Biblia katika nafasi zilizotolewa.*

## KUJIBU KULINGANA NA YALE UYASIKIAYO

Wakati wako umefika wa kutoa uamuzi? Je! Yesu ni mtu fulani wa kihistoria ya kukumbukwa au ni ni Mtu mwenye ziada? Kana ni Mwana wa Mungu, na Muumbaji wa vyote, hauwezi kumwacha. Yesu akasema, “Unafikiri nini juu ya Kristo?” [1] Katika masomo haya tumekuwa tukitafiti juu ya Kristo. Unafikiri nini juu Yake, na utajibu kwa namna gani? Yesu anawataka watu wajibu kwa kutenda mambo na vitu Alivyovisema. Aliwaambia watumie masikio yao na wasiwe wenye kupuuzia, kana kwamba ni viziwi.

Kusikiliza na kutenda

### UNATAKIWA KUJIBU KWA YESU

Kuna matokeo mabaya kwa wale wasiotenda kwa haraka na “kutumia masikio yao”. Soma Mathayo 13:41-43.

Andika mstari wa 43

.....

.....

.....

### WALE WANAOMJIBU NDIO FAMILIA YAKE

Familia ya kweli ya Yesu

Yesu alionya kusikia neno la Mugu na kutolitenda. Aliwahesabia wale watendao mapenzi ya Mungu kuwa familia Yake. Soma Luka 8:19-21.
Andika mstari wa 21

.....

.....

.....

## KUTOKUTENDA HULETA MATESO YA MILELE

Yesu ana wasilizaji wanaotamani – lakini sio wote walioandaliwa kutubu na kukubaliana na mafundisho yake. Walikuwa tayari kukiri na kumwita Bwaba – lakini walishindwa kutenda aliyoyasema. Walimheshimu kwa midomo yao, lakini maisha yao hayakubadilika.

Historia ya nyumba mbili

### UJINGA WA KUMKATAA YESU

Yesu alitumia mfano wa nyumba mbili kuelezea adhari ya kutotenda kulingana na neno Lake. Moja ya nyumba hizi ilijengwa juu ya mchanga, na nyingine mwambani. Upepo na Mafuriko yalizipiga nyumba zote ile

[1] Mathayo 22:42

Kama nitakataa ninakaribisha mabaya

iliyojengwa mwambani ilisimama imara, lakini nyingine iliharibiwa. Wale wamfuatao Yesu ni kama nyumba imara. Soma Luka 6:46-49.

Andika mstari 49

.....

.....

.....

.....

.....

KAMA HATUJAOKOLEWA TUTAANGAMIA

Hukumu ya milele

Kama tukikataa kumfuata Yesu si tu kwamba tunakataa msamaha, ila tunakaribisha uharibifu wa milele – kama mfano uliousoma unavyojieleza kwa wazi. Utaona kutoka kwenye nukuu chini ya karatasi[2] kwamba Yesu aliongea wazi juu ya adhabu/hukumu ya milele. Ulimwengu unaelekea uharibiru.[3] Ni lazima tuwe makini tusiiendee njia sawa na hiyo, bila hivyo tutapata matokeo ya dhambi zetu kama zinavyostahili.

Angalia juu Matendo 2:40

.....

.....

.....

Mbwa mwitu na moto: ishara mbili za Roho wa Mungu

## WAJIBU WETU NA AHADI YA MSAADA WA MUNGU

Wale waliosikia Injili kwanza walitaka kuifuata, lakini hawakujua jinsi ya kuendelea kuishi kama itakavyo. Hivyo waliuliza swali la muhimu sana – "Wanaume na ndugu zetu tufanye nini?". Petro akawaambia tubuni na mkabatizwe. Mtapokea sawasawa, kwa kugeuka kutoka kwenye vitu visivyompendeza Mungu, na mkaonyeshe imani zenu katika Kristo kwa njia ya ubatizo.

Wale wanaotubu na kuamini wameahidiwa msaidizi wa maana sana. Wanaahidiwa zawadi ya Roho Mtakatifu wa Mungu.[4]

YESU ALIAHIDI ROHO MTAKATIFU

Muda mfupi kabla Hajafa, Yesu aliahidi wanafunzi Wake kwamba Mtu mwingine atakuja kuwasaidia. Mtu ni Roho Mtakatifu. Punde tu unapomjua Kristo kama Mwokozi, msaidizi huyu huja kuishi pamoja nawe.

Utakatifu wa wageni

Angalia Yohana 14:16

.....

.....

.....

[2] Luka 16:19-31

[3] Mathayo 7:13

[4] Matendo 2:38 (Uliandika hili katika Somo la 6)

ROHO MTAKATIFU NI MWALIMU WA MKRISTO NA KIONGOZI

Roho wa Mungu anamgawia kila Mkristo kiajabu sana. Maisha ya Ukristo siyo rahisi, lakini yakiwa na Roho Mtakatifu akitufundisha na kutusaidia tunapata nguvu zote tunazohitaji, na hatuwi wapweke. Angalia Yohana 14:26

.....

.....

.....

.....

Msaidizi asiyekoma

ROHO MTAKATIFU ANATUSAIDIA KUOMBA

Moja ya ishara ya kuonyesha kuwa tu Wakristo wa kweli ni uwezo wa kuomba. Roho wa Mungu hututia moyo wa kumwendea Mungu kama Baba yetu, sasa tunakuwa tumepatanishwa Naye kupitia kifo cha Kristo. Angalia Wagalatia 4:6

.....

.....

.....

## KUJIUNGA NA KUKUA

Familia ya Mungu mwenyewe

Je ni kwa jinsi gani waumini wa kanisa la kwanza walivyoipokea Injili? Waliipokea kwa kubatizwa na kujiunga na kanisa. Kiasi cha 3,000 "waliongezeka" katika siku moja! Ilikuwa kawaida kwamba wangejiunga, kama sasa walivyo katika familia moja – familia ya Mungu. Waliendelea kupata nguvu kutoka kwa rafiki zao waliokuwa Wakristo wenye moto.

WALIUNGANA NA FAMILIAYA KANISA

Kama umeingia kwenye imani katika Kriso, unatakiwa kujiunga na kanisa ambalo kwa uaminifu wanafundisha Injili ya Kristo. Unatakiwa kuungana na familia ya Mungu, na kuhudhuria mara kwa mara, kama walivyofanya. Angalia Matendo 2:41

.....

.....

.....

Ushirika

WALIKUA KWENYE FAMILIA

Katika familia yako unakula chakula mara kwa mara ili uendelee kuwa na afya na imara. Kila muumini mpya anahitaji maziwa ya Neno la Mungu ili wakue. Angalia 1 Petro 2:2

.....

.....

Chakula ili ukue

Petro na mitume wengine waliwafundisha hawa Wakristo wa kanisa la kwanza Neno la Mungu. Agano Jipy lina maandishi ya watu hawa. Unatakiwa kuyasoma kila siku na kuyaskikiliza yanavyokueleza. Kwa kufanya hivyo utapokea chakula unachohitaji kukua kuwa Mkristo imara.

WALIKULA CHAKULA CHA KUMBUKUMBU

"Kuvunja Mikate"

Wakristo wa kwanza walichukua mkate na divai kama kumbukumbu ya pasaka. Waliita "Kuvunja Mikate" kwa sababu Yesu alichukua mkate akauvunja, kama mwili Wake uluvyovunjwa. Divai ilikuwa ishara ya damu Yake Alipowafia. Yesu alikuwa ameawaambia kula mkate na kunywa divai kwa kumbukumbu ya kifo Chake cha upendo msalabani.[5] Wakristo wanatakiwa mara kwa mara wanatakiwa kufikiri juu ya upendo wa Yesu kwa kula kwa mfano huu wa chakula cha kawaida na waumini wengine.

Angalia Matendo 2:42

.....

.....

.....

Kujali kwa Mungu kama baba

Angalia jinsi walivyoomba kwa pamoja. Wakiomba pamoja na Wakristo wengine ni chanzo cha uimara wa Kiroho. Kama wewe ni muumini wa kweli katika Kristo hakikisha unaomba mara kwa mara, aidha nyumbani au kanisani. Mungu sasa ni wako mfurahie. Anakujali kama baba, hivyo Mwambie juu ya mahitaji yako lakini pia kumbuka kumshukuru. Angalia Wafilipi 4:6

.....

.....

.....

.....

## NA HITIMISHO

Kuaibika kwa Yesu?

**Kama wewe unadhani ni Mkristo** wa kweli ni lazima usimwonee aibu Yesu.[6] Hakukuonea aibu aliposimama mbele ya serikali ya Rumi (Pontio Pilato)[7] Na alienda msalabani kwa ajili yako.

Hivyo uwe tayari kusema juu ya Yesu kwa wengine. Mungu atakuheshimu, na maisha yako ya kiroho yatazidishwa.

Sasa kwamba umemaliza mafunzo au masomo utatarajia kuchukua yanayofuata katika mtiririko uitwao "Kuanza Kama Mkristo" ambayo yako kwa Kiingereza. Masomo haya ya bure yanaweza kuchukuliwa kwenye mtandao katika tovoti www.biblehelp.co.uk na mtu mwingine mwenye kompiuta. Ongea na kiongozi wako juu ya hili.

[5] Luka 22:19-20

[6] Marko 8:38

[7] 1 Timotheo 6:12-13